**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA 2024/2025

**ILIYOWASILISHWA NA**

**MHE. SHAABAN ALI OTHMAN (MBM)**

**WAZIRI WA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI**

**JUNI, 2024**

# VIONGOZI WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI ZANZIBAR



**Mhe. Shaaban Ali Othman**
**Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi - Zanzibar**



**Captain Hamad Bakari Hamad**
**Katibu Mkuu**
**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi - Zanzibar**



**Nd. Zahor Khamis Mohamed El-kharousy**
**Naibu Katibu Mkuu**
**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi - Zanzibar**



**Ndg. Adam A. Makame**
**Mkurugenzi Mwendeshaji (ZPRA)**



**Ndg. Mikidadi A. Rashid**
**Mkurugenzi Mwendeshaji (ZPDC)**



**Dkt. Salum S. Hamed**
**Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini**



**Dkt. Zakaria A. Khamis**
**Mkurugenzi (ZAFIRI)**



**Dkt. Makame O. Makame**
**Mkurugenzi Idara ya Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari**



**Dkt. Ameir H. Mshenga**
**Mkurugenzi Muendeshaji (ZAFICO)**



**Dkt. Emmanuel A. Sweke**
**Mkurugenzi Mkuu (DSFA)**



**Dkt. Saleh A. S. Yahya**
**Naibu Mkurugenzi (DSFA)**



**Dkt. Salim M. Hamza**
**Afisa Mdhamini (WUBU) PEMBA**



**Ndg. Issa S. Ali**
**Mkurugenzi Idara ya Utumishi na Uendeshaji**



**Ndg. Mohammed S. Khamis**
**Kaimu Mkurugenzi Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.**

# YALIYOMO


Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ..... 1

Utangulizi ..... 1

Ukuaji na Mchango wa Sekta ya Uchumi wa Buluu Katika Pato la Taifa ..... 3

Utekelezaji wa Malengo ya Wizara kwa Mwaka 2023/2024 ..... 7

Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka 2023/2024 ..... 8

Mafanikio ya Mwaka wa Fedha 2023/2024 ..... 9

Utekelezaji wa Programu za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ..... 15

Programu Kuu ya Maendeleo ya Uchumi Wa Buluu ..... 15

Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi ..... 20

Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ..... 29

Changamoto ..... 34

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti inayozingatia Programu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ..... 35

Utekelezaji wa Programu za Wizara ..... 36

Utekelezaji wa Miradi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ..... 36

Malengo ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Kwa Mwaka 2024/2025 ..... 38

Muhtasari wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ..... 53

Hitimisho ..... 54

Viambatisho ..... 58

## HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu lipokee, lijadili, na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa kazi za Kawaida na kazi za Maendeleo, kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ambayo yanawasilishwa katika Mfumo wa Programu (PBB).

2. **Mheshimiwa Spika,** nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uhai na afya njema na kutuwezesha kushiriki katika kikao hiki kinachojadili Bajeti ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

3. **Mheshimiwa Spika,** napenda kutoa shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mchango wake mkubwa anaoutoa kwenye maendeleo ya nchi yetu. Shukurani za pekee zimuendee Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuiongoza Zanzibar katika misingi ya umoja, mashirikiano, usalama, amani na utulivu. Hatua hiyo imepelekea utekelezaji mzuri wa malengo ya Serikali na maelekezo yake anayoyatoa katika kuleta maendeleo ya Sekta za Uchumi wa Buluu na Uvuvi na hatimae kukuza Uchumi wa Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Othman Masoud Othman, Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, na Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, kwa kumshauri vizuri Mheshimiwa Rais wa

Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kufikia azma yake ya kuboresha uchumi na maisha ya Wazanzibari. Vile vile, shukurani za pekee ziende kwa Wajumbe wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwashauri vyema viongozi wetu na kufanya maamuzi mema yenye hekima na busara katika kuleta maendeleo ya Zanzibar.

5. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii adhimu kwa dhati kabisa kukupongeza wewe mwenyewe Mheshimiwa Zubeir Ali Maulid, Spika wa Baraza la Wawakilishi. Pia nawapongeza Naibu Spika, Wenyeviti na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kazi nzuri wanayoifanya na tunawaombea dua Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

6. **Mheshimiwa Spika,** nachukua fursa hii kwa namna ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Mtumwa Peya Yussuf Mwenyekiti wa Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo, pamoja na Wajumbe wote na Sekretarieti ya Kamati hiyo, kwa miongozo na ushauri waliyotoa kwa Wizara katika kufanikisha vizuri utekelezaji wa shabaha na malengo ya bajeti ya mwaka 2023/2024, na kuendelea kutusaidia kufanikisha maandalizi ya bajeti ya Wizara kwa mwaka 2024/2025. Napenda kuihakikishia Kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwamba, maoni, ushauri na mapendekezo mliotupatia yamezingatiwa katika ukamilishaji wa bajeti hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

7. **Mheshimiwa Spika,** kwa dhati kabisa napenda kuchukua fursa hii kumshukuru na kumpongeza aliyekuwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi Kaka yangu Mheshimiwa Suleiman Massoud Makame Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chonga kwa jitihada zake na mchango wake mkubwa aliyoutoa katika kuhakikisha Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inafikia malengo yake iliyojiwekea.

8. **Mheshimiwa Spika,** kwa masikitiko makubwa, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatoa pole kwa watanzania wote kwa vifo vya viongozi wetu wapendwa, aliyekuwa Rais wa awamu ya pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hayati Mheshimiwa Ali Hassan Mwinyi; pamoja na aliyekuwa Waziri Mkuu wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Edward Ngoyai Lowassa. Mwenyezi Mungu awalaze mahala pema Peponi Amiin.

## UKUAJI WA SEKTA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

9. **Mheshimiwa Spika,** Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya awamu ya nane inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi inaendelea na kazi ya kuwawezesha wananchi wa Zanzibar kiuchumi kupitia sekta ya Uchumi wa Buluu. Utekelezaji huu wa majukumu ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi umezingatia maelekezo ya ILANI ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) 2020 – 2025, Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (ZDV) 2050, Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021 – 2026, Malengo ya Maendeleo Endelevu (Agenda 2030) hususan Lengo Namba 14 Mpango wa maendeleo endelevu wa Umoja wa Afrika kupitia lengo nambari 6 pamoja na maelekezo na Ahadi za Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatekeleza kazi zake kupitia Sera ya Uchumi wa Buluu na Mkakati wake wa Utekelezaji, Sera ya Mafuta na Gesi Asilia, Sera ya Uvuvi na Mkakati wake wa Utekelezaji na Sera ya Uvuvi wa Bahari Kuu pamoja na Sheria ya Mafuta na Gesi Asilia, Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar.

10. **Mheshimiwa Spika,** lengo Kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni kuimarisha Matumizi Endelevu ya Bahari

na kuwawezesha Wajasiriamali kwa kuwapatia elimu, uelewa na ufahamu zaidi, ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana za ujasiriamali, uongezaji wa thamani wa mazao ya baharini, upatikanaji wa mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya uvuvi, mazao ya baharini, mwani, biashara za baharini, Utalii, Mafuta na Gesi Asilia na Nishati Mbadala. Katika utekelezaji wa lengo hilo, mkazo zaidi umewekwa katika Uvuvi wa Bahari Kuu maendeleo ya viwanda vya kusarifu samaki, mwani na mazao mengine ya baharini ikiwemo mitambo ya baridi ya kuhifadhia samaki, madiko na masoko ya minada na ujenzi wa bandari jumuishi za uvuvi.

11. **Mheshimiwa Spika,** uzalishaji wa samaki umeongezeka kutoka **tani 61,794** mwaka 2022 zenye thamani ya **Shilingi 391,370,146,212** hadi kufikia tani **80,085** zenye thamani ya **Shilingi 569,079,795,584** kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia **29.5 (Kiambatisho Nam 1)**. Aidha, Uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kutoka tani **12,594** zenye thamani ya **Shilingi 10,054,496,700** mwaka 2022 hadi kufikia tani **16,653** zenye thamani ya **Shilingi 16,514,805,700** mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia **32.2 (Kiambatisho Nam 2)**. Aidha sekta ya Uvuvi imekuwa hadi kufikia asilimia 8.1 kwa mwaka 2023 kutoka asilimia 3.0 mwaka 2022 (OCGS 2023). Ongezeko hili linatokana na hatua mbalimbali za Serikali katika kuimarisha sekta ya Uvuvi kwa kuwewezesha wavuvi, wakulima wa mwani na wafugaji wa mazao ya baharini kwa kuwapatia nyenzo za kisasa, masoko na kuimarisha usimamizi wa hifadhi za bahari.

12. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imekamilisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar ambayo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Vilevile, Wizara imezindua rasmi Sera ya

Uchumi wa Buluu pamoja na Mkakati Wake wa Utekelezaji, Sera ya Uvuvi pamoja na Mkakati Wake wa Utekelezaji, Mpango Mkuu wa Uvuvi, pamoja na Mkakati wa Utekelezaji wa Ukondoishaji Masuala ya Kijinsia katika Uchumi wa Buluu (Gender Action Plan on Blue Economy), Tafsiri ya Kiswahili ya Sera ya Uvuvi ya Zanzibar; Mpango Kazi wa Utekelezaji wa FAO kwa Wavuvi Wadogo Wadogo pamoja na Mpango Mkakati wa Kitaasisi wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

13. **Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio hayo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imefanya kazi kubwa ikishirikiana na "Zanzibar Marine Hatchery Company Limited" Iliyopo Beit-el-Ras ambayo Wizara ina hisa ya asilimia 45 na Shirika la Mwambao Coastal Comunity kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa vifaranga vya majongoo bahari. Ambapo upatikanaji wa vifaranga hivyo unatarajiwa kuanza hivi karibuni. Vilevile, Wizara kupitia ZAFICO iliweka Jiwe la Msingi katika Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa kilichopo eneo la Kama Unguja. Miundombinu hiyo itatoa mchango mkubwa katika kuendeleza biashara na huduma muhimu kwa wavuvi na wananchi kwa ujumla katika sekta ya Uchumi wa Buluu.

14. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio makubwa yanaendelea kupatikana katika Sekta ya Uchumi wa Buluu ambapo katika utekelezaji wa programu ya UVIKO 19, jumla ya Boti **1,027** zimetengenezwa na boti **987** (**361** – Unguja na **626** Pemba) tayari zimegaiwa kwa wananchi. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa mashamba **100** ya ufugaji wa majongoo bahari (Unguja 50 na Pemba 50), mashamba **60** ya ufugaji wa Kaa (30 Unguja na 30 Pemba) na mabwawa **20** ya ufugaji wa samaki (10 Unguja na 10 Pemba). Aidha, Mafunzo kwa wajasiriamali wa sekta ya Uvuvi, wafugaji wa mazao ya baharini na wakulima wa mwani yametolewa, ambapo jumla ya wajasiriamli **4,000** wamepatiwa mafunzo hayo. Vilevile,

mafunzo maalum ya matumizi ya vifaa vya vitafuta samaki (fish finder) na GPS Receiver yametolewa kwa walimu **70** na wavuvi **665** (**405** - Unguja na **260** - Pemba).

15. **Mheshimiwa Spika,** kimbunga Hidaya, ambacho kilipiga Zanzibar mnamo tarehe 3 hadi 5 Mei, 2024 kikiwa na nguvu za upepo wa kasi ya Kilomita 150 kwa saa, kimeathiri jumla ya vyombo 214 vya Uvuvi vyenye thamani ya **Shilingi 850,000,000.** Aidha, Wizara tayari imeanza mazungumzo ya awali na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) kuhusu kuwapatia mkopo wavuvi walioathirika vyombo vyao na Kimbunga hicho.

16. **Mheshimiwa Spika,** kazi ya matayarisho ya Mpango Maalumu wa Upangaji maeneo ya Bahari "Marine Spatial Planning" inaendelea, ambapo tayari imekamilisha zoezi la upembuzi wa awali "Scoping study on the status of Marine Spatial Planning in Tanzania the United Republic of Tanzania" wa kutazama utayari wa kuendelea na mchakato wa MSP nchini. Aidha, muongozo wa Mpango wa Matumizi ya Bahari katika Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania tayari umekamilika. Sambamba na haya, hatua mbalimbali zinazohusiana na MSP zimekuwa zikiendelea nchini ikiwemo mafunzo ya "ITP-MSP Training" yanayofadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Swiden (SIDA) na kutekelezwa na Sweedish Agency for Marine and Water Management". Vile vile, Ofisi ya Makamu wa kwanza wa Rais kupitia mradi wa "Sapphire Project" unaofadhiliwa na Taasisi ya Shirika la Umoja wa Mataifa kupitia Nairobi Convetion imefanya kazi ya majaribio ya Upangaji wa Maeneo ya Bahari (MMSP) katika eneo namba 3 la Hifadhi ya bahari ya PECCA Kisiwani Pemba.

17. **Mheshimiwa Spika,** katika sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, mafanikio makubwa yamefikiwa kufuatia uzinduzi wa duru ya kwanza ya utoaji wa vitalu vya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar. Wizara kwa kushirikiana na Kampuni ya SLB na na Frontier Energy Network za Uingereza imeanza zoezi hilo

na tarehe 20 Machi, 2024 Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi alizindua rasmi.

18. **Mheshimiwa Spika,** Wizara imesimamia kazi ya kufanya malipo kwa wananchi walioathiriwa na mzozo wa wavuvi wa vijiji vya Chwaka na Marumbi mwaka 1996 ambapo wananchi 18 waliothibitishwa (verified) wamelipwa jumla ya **Shilingi 50,269,000**. Halikadhalika, jumla ya **Shilingi 744,786,000** ambazo ni fidia za waathirika wa ujenzi wa miradi wa Maendeleo eneo la Ndagoni Pemba, Fungurefu, Bwereu pamoja na Kama kwa upande wa Unguja tayari zimeshalipwa.

**UTEKELEZAJI WA MALENGO YA WIZARA KWA MWAKA 2023/2024**

19. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imesimamia utekelezaji ILANI ya Uchaguzi ya CCM, malengo ya Dira ya 2050, Mpango wa Maendeleo Zanzibar (ZADEP), Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs), pamoja na Sera na Mipango Mikakati ya Kisekta ya Uchumi wa Buluu. Utekelezaji wa Mikakati na Malengo hayo kumepelekea kuongezeka kwa taaluma na teknolojia kwa wavuvi, wakulima wa mwani, na wafugaji wa mazao ya baharini. Aidha, mikakati hiyo imesaidia kujenga uelewa kwa taasisi za Serikali na sekta binafsi kuhusu uwekezaji na uwezeshaji katika sekta ya Uvuvi, Mwani, Mazao ya Baharini, Utafiti, uhifadhi wa maeneo ya bahari, na Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

20. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 imetekeleza malengo yake kupitia Programu Kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu

ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

21. **Mheshimiwa Spika,** kupitia programu hizo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilipanga kutekeleza jumla ya Miradi kumi na saba (17) **(Kiambatisho Nam. 3)**.

**MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2023/2024**

22. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imekadiriwa kukusanya Mapato ya jumla ya **Shilingi 5,727,275,209** kutoka vianzio vyake 4 vya Unguja na Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, Wizara imekusanya jumla ya **Shilingi 4,062,433,231** sawa na asilimia **70.9** ya makadirio (**Kiambatisho Nam.4**).

23. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2023/2024 iliidhinishiwa kutumia jumla ya **Shilingi 81,061,012,171** Kati ya fedha hizo **Shilingi 9,313,000,000** kwa Kazi za Kawaida na **Shilingi 71,748,012,171** kwa Kazi za Maendeleo.

24. **Mheshimiwa Spika,** mgawanyiko wa fedha kwa Kazi za Kawaida ni **Shilingi 9,313,000,000;** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 3,814,300,000** Mishahara, **Shilingi 2,452,400,000** kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 3,046,300,000** ni Ruzuku kutoka SMZ (**Shilingi 240,000,000** ni kwa ajili ya ZAFIRI, **Shilingi 2,378,200,000** ni kwa ZPRA na **Shilingi 428,100,000** ni kwa ZAFICO).

25. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi, 2024, fedha zilizopatikana ni **shilingi 8,639,027,628** sawa na asilimia **10.6** ya fedha zilizopangwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 6,013,213,930** ni kwa ajili ya kazi za kawaida, ambapo **Shilingi 716,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, **Shilingi 3,207,811,972** ni Mishahara na **Shilingi**

**2,089,401,958** ni Ruzuku kutoka SMZ ambapo **Shilingi 501,392,333** kwa ajili ya matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 1,588,009,625** ni Mishahara.

**26. Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Wizara imeingiziwa jumla ya **Shilingi 2,625,813,698** sawa na **asilimia 3.7** Ambapo **Shilingi 2,184,043,802** kutoka SMZ kwa kuimarisha Sekta ya Uvuvi na **Shilingi 441,769,896** kutoka Washirika wa Maendeleo (**Kiambatisho Nam. 5**).

## MAFANIKIO YA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

**27. Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Julai hadi Machi 2023/2024, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ilitekeleza programu zake kwa ufanisi na kupata mafanikio yafuatayo:

i. Kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji wa samaki kutoka tani **61,794** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 391.37** kwa mwaka 2022 hadi kufikia tani **80,085** zenye thamani ya **Shilingi Bilioni 569.07** kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia **29.5.** Vile vile, Uzalishaji wa zao la mwani umeongezeka kutoka tani **12,594** zenye thamani ya **Shilingi 10,054,496,700** kwa mwaka 2022 hadi kufikia tani **16,653** zenye thamani ya **Shilingi 16,514,805,700** kwa mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia **32.2.**

ii. Wizara imekamilisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini ambayo imepitishwa na Baraza la Wawakilishi na kusainiwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Aidha, Wizara imefanya marekebisho ya Sheria ya Mafuta na Gesi ili kuvutia uwekezaji zaidi na marekebisho hayo yalipitishwa na Baraza la Wawakilishi.

iii. Utangazaji wa Vitalu vinane (8) Vipya vya Mafuta na Gesi Asilia vilivyopo katika maeneo ya Bahari ya Zanzibar

umetekelezwa kwa mashirikiano na Kampuni za SLB pamoja na Frontier Enery Network ya Uingereza na umezinduliwa rasmi na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, tarehe 20 Machi, 2024. Vilevile, Wizara imekamilisha marekebisho ya Modeli ya makubaliano ya mgawanyo wa uzalishaji "Model of Production Sharing Agreement (MPSA)". Pamoja na kuanzisha kituo cha muda cha kuhifadhia taarifa za Mafuta na Gesi Asilia. Wizara ipo katika hatua za mwisho za kukitangaza upya Kitalu cha Pemba-Zanzibar baada ya kuvunja Mkataba wa awali na Kampuni ya RAKGas.

iv. Katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia, kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Udhibiti wa Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA), Serikali imefanya malipo ya fidia kwa wananchi walioathiriwa mali zao wakati wa zoezi la mtetemo, ambapo jumla ya wananchi 3,575 walilipwa kati ya wananchi 4,330 waliothibitishwa (verified) kulipwa. Utekelezaji huu ni sawa na asilimia **82.6** ya malengo yaliyowekwa. Jumla ya **Shilingi 1,200,000,000** zimelipwa kati ya **Shilingi 1,300,000,000** zilizotengwa ambazo ni wastani wa **asilimia 92.3** ya fedha ambazo wananchi walioathirika na utafiti wa awali wa Mafuta na Gesi Asilia. Wananchi wachache waliobakia wanatarajiwa kulipwa hivi karibuni.

v. Katika Maadhimisho ya Miaka 60 ya Sherehe za Mapinduzi ya Zanzibar, Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mwambao Coaster Community, imezindua Kituo cha Kijamii cha kutotolesha Vifaranga vya Majongoo bahari Pujini Pemba. Aidha, Wizara kupitia Kampuni ya ZAFICO iliweka Jiwe la Msingi katika Ujenzi wa Kiwanda cha Kusarifu Dagaa kilichopo eneo la Kama Unguja.

vi. Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya "Wildlife Conservation Society" imekamilisha utafiti wa kuangalia

"Biodiversity Value and Current Ecological Condition on Marine and avifauna" katika kisiwa cha Latham.

vii. Wizara kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (IFAD) umefanikiwa kufundisha wakufunzi (TOT) 95 (Unguja 31 na Pemba 64) wanaotarajiwa kufundisha wakulima wa mwani teknolojia mpya ya kilimo cha mwani cha maji marefu. Aidha, Programu hii imefanikiwa kuandaa muongozo wa kufundishia kilimo cha mwani cha maji marefu na uongezaji wa thamani.

viii. Wizara kupitia Programu ya kuendeleza Kilimo na Uvuvi imekamilisha tathmini ya athari ya kimazingira (ESIA) ya Uvuvi ya Bahari Kuu na Kiwanda cha Kusarifu samaki Fungu Refu. Vile vile, Wizara inatarajia kupokea Ripoti ya upembuzi yakinifu "Feasibility Study" ya ununuzi wa meli za Uvuvi mwezi wa Juni 2024. Kiwanda cha kusarifu samaki na taratifu za uendeshaji wa meli na Kiwanda kwa mfumo wa PPP. Aidha timu ya ununuzi wa meli inayojumuisha wajumbe 12 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar imeundwa na taratibu za manunuzi ya meli zinatarajiwa kuanza mapema mnamo mwezi Julai 2024. Awali Programu ilipanga kununua meli nne (4) za mita 18 zenye thamani ya **Shilingi 5,442,880,000.** Baada ya mazingatio ambayo yametokana na uzowefu tulionao wa meli kama hizo za mita 18 za ZAFICO, Wizara imeona ni vyema tukawa na meli kubwa ya mita 25 inayoweza kuleta tija zaidi katika uvuvi wa Bahari Kuu. Idadi ya meli zitakazonunuliwa inategemea na matokeo ya ripoti upembuzi yakinifu.

ix. Vile vile Wizara kupitia Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi imekamilisha Upembuzi yakinifu "Feasibility Study" ya ununuzi wa meli na Ujenzi wa Kiwanda cha kuchakata samaki kwa lengo la kuendelea na hatua za manunuzi.

x. Wizara tayari imeanza utekelezaji wa Mradi wa **"Integrated Mariculture Value Chain for Women Empowerment in Zanzibar** utakaojenga viwanda vya kusarifu mwani Unguja na Pemba pamoja na kuanzisha mashamba manne (4) ya majaribio ya mwani na majongoo bahari. Aidha, watendaji kumi na tatu (13) wa Wizara wamepata fursa ya kushiriki mafunzo ya muda mfupi ya uzalishaji wa kaa, majongoo bahari, samaki aina ya mwatiko (milk fish) pamoja na utengezaji wa chakula cha samaki katika Chuo Kikuu cha Pukyong nchini Korea.

xi. Korea tayari imesharidhia kuanza kwa upembuzi yakinifu wa ujenzi wa bandari za uvuvi katika maeneo ya Shumba Mjini, Mkokotoni Fungurefu, na pia upembuzi wa bandari ya kutengeneza meli (Shipyard) katika eneo la Mangapwani.

xii. Utekelezaji wa ukondoishaji wa masuala ya Mpango makhsusi wa Matumizi ya Bahari (Marine Spatial Planning) kupitia Idara ya Maendeleo ya Uratibu wa Uchumi wa Buluu unaendelea kwa mashirikiano ya karibu na Ofisi ya Makamo wa Rais SMT na tayari muongozo wa jinsi ya kufanya mchakato wa mpango huu umekamilika. Pia watendaji ambao watahusika kuufanyia kazi mpango huu kutoka taasisi mbali mbali za Serikali wanaendelea kupata mafunzo yanayoendelea kufadhiliwa na Serikali ya Sweden.

xiii. Wizara ilikuwa ni mwenyeji wa mafunzo ya kikanda ya MSP yaliyofanyika Zanzibar na kushirikisha nchi takribani zote za ukanda wa Magharibi ya Bahari ya Hindi. Aidha; Wizara imeshirikiana na Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kufanya zoezi la majaribio la MSP katika eneo la Zone 3 katika hifadhi ya mkondo wa Pemba (PECCA).

xiv. Utekelezaji wa Hati ya Mashirikiano baina ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Zanzibar na Wizara inayosimamia masuala ya bahari ya Ufaransa, unaendelea ambapo Ufaransa imemleta Mtaalamu wa Masuala ya Usalama wa Bahari ambae anaendelea kusaidia kuwekeza katika mbinu na mafunzo ya Usalama wa baharini kwa KMKM. Pia Wataalamu kutoka World Maritime Cooperation ya Uholanzi wanatarajia kuingia MoU na Wizara katika uanzishwaji wa Chuo cha Ubaharia. Vilevile, Wizara imepata baraka kutoka Baraza la Mapinduzi ya kuanzisha Chuo hicho cha Uvuvi hapa Zanzibar.

xv. Wizara kupitia Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar imesaini hati ya mashirikiano na Taasisi ya Utafiti ya China (Second Institute of Oceanography) katika kufanya tafiti za Bahari na kujenga uwezo wa wataalamu, ambapo watendaji wanne wameshiriki mafunzo ya "Marine Observation" nchini China.

xvi. Utekelezaji wa Hati ya Makubaliano na Kampuni ya Evergreen Egypt United ya Misri, kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya uvuvi wa bahari kuu, kuanzisha viwanda vya kusarifu samaki pia kufanya ufugaji wa mazao ya Baharini Zanzibar, unaendelea, na kufuatia ziara ya ujumbe wa Wizara nchini Misri Mwezi wa Novemba mwaka 2023, awamu ya kwanza ya uletaji wa Meli za Uvuvi pamoja na Ujenzi wa Viwanda kwa mashirikiano na ZAFICO katika eneo la Kama ipo katika matayarisho. Aidha, Kampuni ya Evergreen na ZAFICO zinatarajia kusaini Mkataba wa Makubaliano ya Kibiashara mwaka 2024.

xvii. Utekelezaji wa mashirikiano na Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID) kupitia Kampuni ya Chemonics International ambayo inatekeleza Mradi mpya wa Uchumi wa Buluu wa "Heshimu Bahari", unaendelea kupitia shughuli mbali mbali ikiwemo uwezeshaji wa wanajamii na wataalamu.

xviii. Utekelezaji wa Mkataba baina ya Wizara (kupitia Idara ya Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari) na Kampuni ya &Beyond Tanzania inayoendesha shughuli za utalii (hoteli) katika kisiwa cha Mnemba kuhusu uhifadhi wa Eneo Mahsusi kuzunguka kisiwa cha Mnemba, unaendelea.

xix. Kuwasili kwa mtambo wa kuzalisha vinoo vya barafu wenye uwezo wa kutoa tani tano (5) sawa na vinoo sabini na mbili (72) zenye kilo 18 kutoka Kampuni ya Albacora ya Hispania ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mkataba wa uvuvi wa kampuni hiyo na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu. Mtambo huu tayari unafanya kazi na upo katika Diko na Soko la Samaki Malindi.

xx. Miongozo ya utalii wa Pomboo, Kiti cha pweza na matumbawe pamoja na uhifadhi wa Kasa imeandaliwa kwa lengo la kuisambaza kwa walengwa ili kuwa na utalii unaozingatia uhifadhi wa mazingira. Aidha, Wizara inaendelea kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuhifadhi Kasa na athari za kula Kasa kwa Jamii.

xxi. Katika juhudi za Wizara za kupambana na Uvuvi haramu katika maeneo ya karibu na Fukwe na Hifadhi, jumla ya doria shirikishi 220 zilifanyika Unguja na Pemba katika maeneo yote ya hifadhi za bahari kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu (Nyavu za macho madogo, bunduki na madema ya waya) unaopelekea uharibifu wa mazingira ya bahari. Aidha, vyombo 47 vilikamatwa vikivua Uvuvi usiokubalika katika hifadhi za bahari. Ambapo kesi zao zilihukumiwa nje ya Mahakama kwa kupewa elimu ya uhifadhi na wengine kulipa faini.

xxii. Maeneo 2 yamewekewa matumbawe bandia, Maeneo 4 ya ufungaji wa miamba ya Pweza na samaki wa miambani yamefunguliwa na maeneo 8 tengefu ya miamba ya kudumu yamefungwa ili kuboresha afya ya bahari. Maeneo tengefu ya kudumu ni Uroa, Michamvi, Ukongoroni, Marumbi, Mtende, Fundo, Gando na Kukuu

na maeneo mawili ya Mnemba na Jambiani yamewekwa matumbawe bandia na kazi ya ufuatiliaji inaendelea.

xxiii. Wizara kwa kushirikiana na Shirika la Mwambao imetoa boti mbili za mita 8 kwa maeneo ya Uhifadhi shirikishi. Vilevile, Shirika la The Nature Conservancy (TNC) imetoa boti mbili za mita nane kwa wakulima wa mwani wa Muungoni na Tumbe.

**UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024**

**28. Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa shabaha za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kupitia Programu zake kuu tatu(3) na Programu ndogo sita (6) ni kama ifuatavyo;

**PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU**

**29. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu dhumuni lake kubwa ni Kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Programu hii ina programu ndogo moja nayo ni Maendeleo ya Uchumi wa Buluu na ina huduma mbili kama ifuatavyo:

i. Uratibu wa Uchumi wa Buluu

ii. Udhibiti wa ufuatiliaji na uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

**30. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii iliombewa **Shilingi 17,147,383,200.** Kati ya hizo **Shilingi 167,083,200** ni Mishahara, **Shilingi 602,100,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 2,378,200,000** ni Ruzuku kwa ZPRA. Matumizi ya fedha za Ruzuku za ZPRA ni kama ifuatavyo: **Shilingi 1,498,300,000** ni Mishahara na **Shilingi 879,900,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Aidha Programu ya Maendeleo ya Uchumi

wa Buluu imepangiwa kutumia **Shilingi 14,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 6,000,000,000** ni kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Bahari Maisha na **Shilingi 8,000,000,000** ni kwa ajili ya Programu ya Mafuta na Gesi Asilia.

31. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2024, Programu hii imepata jumla ya **Shilingi 1,770,180,622** sawa na asilimia **10.3.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 66,832,723** kwa Matumizi ya Kawaida ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 1,703,347,899** ni RUZUKU kwa ZPRA.

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU.

32. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu uwezeshaji, uongezaji thamani na kuimarisha masoko ya bidhaa za Mazao ya Baharini;

ii. Kuratibu na Kushiriki katika Matamasha, Mikutano ya Uwekezaji na Uwezeshaji wa Uchumi wa Buluu Kitaifa, kikanda na Kimataifa;

iii. Kutoa uelewa wa dhana ya Uchumi wa Buluu na vipaumbele vyake kwa umma, pamoja na wafanyakazi wa Taasisi mbalimbali za Serikali pamoja na sekta binafsi ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Kinondoni Dar es Salaam, Ujumbe kutoka Jiji la Tanga, Afrika ya Kusini, Maafisa na Wanachama wa Nchi za Kusini mwa Bara la Afrika (SWIO), Abu Dhabi, ZBS na ZEEA;

iv. Idara imetoa mafunzo juu ya uhusiano uliopo baina ya Uchumi wa Buluu na uhifadhi wa mikoko kwa Wajumbe wa Ngazi za juu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakiwemo Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama vya Mkoa wa Tanga, Pwani na Wilaya zake.

v. Kukamilika kwa muongozo wa uandaaji wa MSP kwa Tanzania na kuchapishwa katika tovuti ya Ofisi ya Makamu wa Rais wa Tanzania mwezi Oktoba, 2023. Muongozo huu unatoa maelekezo ya namna ya kuendesha mchakato mzima wa MPS Tanzania.

vi. Mchakato wa kuandaa Mpango Mkakati wa mawasiliano wa MSP umekamilika na upo katika hatua ya kuombewa fedha.

33. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu iliombewa Jumla ya **Shilingi 6,769,183,200.** Kati ya hizo **Shilingi 167,083,200** ni Mishahara, **Shilingi 602,100,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 6,000,000,000** ni kwa ajili ya Utekelezaji wa Mradi wa Bahari Maisha. Hadi kufikia Machi 2023, Programu hii imepatiwa jumla ya **Shilingi 66,832,723** sawa na asilimia **1.**

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA (ZPRA)**

34. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia ni taasisi yenye jukumu la kusimamia na kudhibiti shughuli zote za Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

35. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii ilitekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kusimamia mpango wa ugawaji wa vitalu vipya utafutaji wa Mafuta na Gesi asilia na kukabidhi Ripoti ya Kitaalamu Serikalini. Aidha, Mamlaka imefanikiwa kuandaa Mkakati wa Utangazaji (Licencing Round Strategic) Kufanya marekebisho ya Modeli ya Mkataba wa PSA (MPSA), kuandaa na kuingia Mkataba na Kampuni ya Frontier Energy Network kwa lengo la kuvinadi vitalu husika katika soko la Kimataifa.

ii. Wizara imefanikiwa kuendesha duru ya awali ya kutangaza utoaji wa vitalu 8 (The first licensing round) kwa ajili ya uwekezaji katika shughuli za utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia ambapo uzinduzi rasmi wa zoezi hili ulifanywa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi tarehe 20 Machi 2024.

iii. Wizara imefanikiwa kuendelea na zoezi la kusimamia ulipaji wa fidia kwa Wananchi 975 kwa mwaka wa fedha 2023-2024.

iv. Mamlaka imeshiriki makongamano mawili (2) yaliyofanyika nchini Norway kupitia ufadhili wa Shirika la Nerwegian Petroleum Directorate (NPD) na Dar-es-Salaam, Pia kushiriki mafunzo ya muda mfupi 12. Aidha mfanyakazi mmoja amejiunga mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya Shahada ya Pili Nchini Norway.

iv. Jumla ya Programu 29 zimeendeshwa kupitia Mikutano ya hadhara, Mikutano ya Taasisi, makongamano pamoja na vyombo vya habari zikilenga kujenga uwelewa kwa Jamii kuhusiana na masuala ya Mafuta na Gesi asilia.

v. Mikutano miwili (2) ya kujadili utekelezaji wa maeneo ya Kimkakati yaliyoainishwa katika hati ya makubaliano kwa kipindi cha utekelezaji wa robo ya kwanza na ya pili ya mashirikiano ya Kisekta baina ya Mamlaka za ZPRA na PURA.

**36. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) iliombewa jumla ya **Shilingi 6,378,200,000.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 1,498,300,000** ni Mishahara na **Shilingi 879,900,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 4,000,000,0000** ni kwa kutekeleza mradi wa maendeleo (NDR). Hadi kufikia Machi 2024, Mamlaka imepatiwa **Shilingi 1,703,347,899** sawa na asilimia **26.71.** Kati ya Fedha hizo

**Shilingi 1,294,605,899** ni Mishahara na **Shilingi 408,742,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPDC).**

**37. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar imelenga kuendeleza utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa kampuni. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia imeweza kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kutafsiri taarifa za Kitalu cha Pemba - Zanzibar kwa kushirikiana na Mjiolojia mstaafu wa Shirika la Maendeleo la Petroli Tanzania (TPDC) pamoja na kuandaa mkakati wa uendelezaji wa Kitalu hicho baada ya kumalizika kwa Mkataba baina ya Serikali na Mkandarasi RAK Gas.

ii. Kuandaa Mpango Kazi na Bajeti (Work Program and Budget) ya 3D ya eneo la Kitalu cha Pemba – Zanzibar kwa lengo la kuliendeleza baada ya kumalizika kwa Mkataba baina ya Serikali (SMZ) na Mkandarasi RAK Gas ili kuweza kupata shughuli zitakazohitajika na gharama zake.

iii. Kampuni inaendelea na juhudi za kumtafuta mbia atakaeweza kujenga Bohari za kuhifadhia Mafuta na Gesi asilia kwa kushirikiana na ZPDC.

iv. Mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi yamefanyika kwa Wataalamu ili kuwajengea uwezo ikiwemo uwekezaji wa mkondo wa chini katika Mafuta na Gesi asilia ikijumuisha gesi ya “LNG”, mkondo wa chini (Downstream), mafunzo ya “BOSIET” pamoja na ziara ya kimafunzo nchini India na Oman.

v. Kampuni kwa kushirikiana na Mamlaka ya ZPRA, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilifanya mazungumzo na Kampuni ya RAKGas kupitia vikao mbalimbali na imefanikisha kuvunja Mkataba wa PSA baina ya Kampuni ya RAKGas na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kusaini "Deed of Termination".

vi. ZPDC kwa kushirikiana na ZPRA kwa sasa wanaandaa mpango wa kuendeleza Block lililokuwa chini ya RAK Gas.

vii. Kampuni iliandaa Kongamano la Kimataifa la Sekta ya Nishati kwa kushirikiana na Kampuni ya GEP kutoka Nchini Uingereza, lengo la Kongamano ni kuitangaza na kuifungua Zanzibar kimataifa katika masuala ya Mafuta na Gesi Asilia.

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar iliombewa jumla ya **Shilingi 6,500,000,000.** Kati ya hizo **Shilingi 2,500,000,000** kwa ajili ya Uendeshaji wa Kampuni na **Shilingi 4,000,000,000** kwa kutekeleza miradi ya maendeleo. Ambapo **Shilingi 3,000,000,000** kwa kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Bidhaa za Petroli iliyosafishwa na Usambazaji na **Shilingi 1,000,000,000** kwa kutekeleza Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Gesi Asilia na Miundombinu ya Usambazaji wa Gesi. Hadi kufikia Machi 2024, Kampuni ilipatiwa **Shilingi Bilioni 1,547,000,000** sawa na asilimia **23.8.** Ambapo **Shilingi Bilioni 1,240,000,000** ni Mishahara na **Shilingi Milioni 307,000,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

**39. Mheshimiwa Spika,** Programu kuu ya Maendeleo ya Uvuvi imegawika katika programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa mazao ya baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari;

40. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi 57,513,841,671.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 3,265,829,500** ni kwa Matumizi ya Kawaida ambapo, **Shilingi 1,886,533,500** ni Mishahara, **Shilingi 711,196,000** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, na **Shilingi 668,100,000** ni Ruzuku (**Shilingi 240,000,000** kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Baharini - ZAFIRI na **Shilingi 428,100,000** kwa ajili ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar - ZAFICO). Katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo Programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi 54,248,012,171.** Kati ya hizo **Shilingi 27,500,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 26,748,012,171** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

41. **Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia Machi 2024 programu imepata jumla ya **Shilingi 4,935,968,412** sawa na asilimia **8.58** Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,310,154,714** kwa Matumizi ya Kawaida. Ambapo **Shilingi 1,726,139,164** Mishahara, **Shilingi 197,961,491** kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 386,054,059** ni Ruzuku. Katika kutekeleza miradi ya Maendeleo Programu hii imepatiwa **Shilingi 2,625,813,698** (**Shilingi 2,184,043,802** kutoka SMZ na **Shilingi 441,769,896** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. (**Shilingi 44,395,010** kutoka Shirika la NORAD kwa kutekeleza Mradi wa Samaki, **Shilingi 87,896,377** kutoka Shirika la FAO kwa kutekeleza Mradi wa SWIOFC, na **Shilingi 309,478,509** kutoka Shirika la IFAD kwa kutekeleza Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi).

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UVUVI NA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza uvuvi na kuongeza

uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu ndogo hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendeleza taratibu za ununuzi wa meli za kisasa kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi - IFAD.

ii. Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu samaki katika eneo la Fungurefu - Mkokotoni kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi - IFAD.

iii. Ujenzi wa mitambo ya baridi kupitia mfumo wa umeme wa jua kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi - IFAD.

iv. Makampuni 12 yanayojihusisha na usafirishaji wa mazao ya baharini kwenda nchini China yameshapatiwa ruhusa ya kupeleka mazao ya baharini moja kwa moja kutoka Zanzibar.

v. Wakulima 82 (63 wanawake na wanaume 19) wameandaliwa na kupatiwa elimu ya walimu wa walimu (TOT) ili kuongezewa wigo wa walimu wenye taaluma ya kilimo cha mwani watakaosaidia utaalamu na usimamizi kwa wakulima wapya na wa zamani.

vi. Wakulima 350 wamepatiwa vifaa vya kilimo cha mwani ikiwemo kamba, taitai na boti kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mwani.

vii. Kutoa taaluma ya Uvuvi endelevu na wenye tija kwa kamati 91 za Uvuvi Unguja na Pemba.

43. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Programu ndogo hii iliombewa jumla ya **Shilingi 47,575,426,971.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,254,393,500** kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 1,886,533,500** ni Mishahara na **Shilingi 367,860,000** ni kwa matumizi ya

uendeshaji ya ofisi. Katika kutekeleza miradi ya maendeleo programu hii iliombewa jumla ya **Shilingi 45,321,033,471.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 23,500,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 21,821,033,471** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024 programu hii imepata jumla ya **Shilingi 4,850,589,768** sawa na asilimia **9.06.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,224,776,070** kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo **Shilingi 1,726,139,164** ni Mishahara na **Shilingi 112,582,847** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Katika Kutekeleza miradi ya Maendeleo Programu hii imepatiwa **Shilingi 2,493,522,311** (**Shilingi 2,184,043,802** kutoka SMZ na **Shilingi 309,478,509** kutoka kwa Shirika la Maendeleo - IFAD).

**TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR - ZAFIRI**

**44. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Malisili za Baharini Zanzibar imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Tafiti mbili zimefanyika. Ripoti moja ya utafiti tayari imekamilika kwa ajili ya kutoa taarifa ya utafiti huo kwa wadau husika wakiwemo wavuvi. Aidha, Ripoti ya pili inaendelea kupitiwa na watafiti husika.

ii. Miongozo miwili ya kufanya uchunguzi wa kimaabara imetengenezwa katika hatua za awali ambayo ni; Muongozo wa uchunguzi wa bidhaa ya Dagaa na Muongozo wa uchunguzi wa minyoo katika Samaki.

iii. Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Baharini kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi – IFAD inaendelea na taratibu za uanzishwaji wa maabara ya uzalishaji wa mbegu bora za mwani ‘Tissue Culture’.

iv. Taasisi kwa kushirikiana na Kampuni ya Afrivision kupitia Kampuni ya pamoja ya Zanzibar Marine Hatchery

Company Ltd inaendelea kuzalisha vifaranga vya Majongoo bahari. Aidha, uzalishaji wa vifaranga vya kaa tope na samaki wa Mwatiko bado haujaanza. Kwa sasa Kampuni imeweka nguvu katika uzalishaji wa vifaranga vya Majongoo bahari.

45. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar imeombewa jumla ya **Shilingi 5,014,832,528.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 240,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 4,774,832,528** ni kwa utekelezaji wa kazi za Maendeleo ambapo **Shilingi 4,000,000,000** kutoka SMZ na **Shilingi 774,832,528** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024 Taasisi imepata jumla ya **Shilingi 224,941,720** sawa na asilimia **4.49** ya fedha zilizopangwa. Kati ya fedha hizo **Shilingi 92,650,333** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 132,291,387** ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo ambapo **Shilingi 44,395,010** kwa kutekeleza Mradi wa Samaki (NORAD) na **Shilingi 87,896,377** kwa kutekeleza Mradi wa SWIOFC (FAO).

## KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR – ZAFICO

46. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kampuni ya Uvuvi Zanzibar inaendelea na ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la KAMA.

ii. Kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi watakaothirika katika ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki Fungurefu Mkokotoni. Tathmini ya athari za kimazingira na kijamii kuhusiana na mradi imekamilika.

iii. Kushirikiana na sekta binafsi katika kuendeleza uvuvi na ufugaji wa kisasa wa mazao ya baharini (samaki na

Kamba) kutoka Shirika la Maendeleo la KOICA. Mradi huu unafanyika Kizimkazi - Unguja kwa majaribio, ambapo mradi mkubwa unatarajiwa kufanyika Kiungoni - Pemba.

iv. Kuendelea na matayarisho ya ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu Samaki Shumba Mjini kwa upande wa Pemba. Hati miliki ya eneo pamoja na tathmini ya mali na mazao ya wananchi yaliopo katika eneo hilo tayari imepatikana.

v. Kuendelea na matayarisho ya Ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki na mitambo ya baridi kitakachojengwa Fungurefu- Mkokotoni kupitia mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi – IFAD.

vi. Kukamilisha mchakato wa upembuzi yakinifu "Feasibility Study" kwa ajili ya ununuzi wa meli na Ujenzi wa Kiwanda cha kuchakata samaki na mitambo ya baridi.

vii. Kuanza hatua za awali za ujenzi wa kituo cha kusarifu dagaa Ndagoni - Pemba ikiwemo upatikanaji wa hatimiliki Michoro ya ujenzi wa miundombinu pamoja na malipo ya fidia za wananchi waliothirika mali na mazao katika eneo la mradi zimekamilika.

viii. Kampuni ya ZAFICO iliingia mkataba na Kampuni ya Blue Land kwa ajili ya ukodishwaji wa boti za Uvuvi (Sehewa 2 na Sehewa 3). Hata hivyo, Kampuni ya Blue Land imeshindwa kukamilisha makubaliano hayo kwa kushindwa kuwasilishwa malipo ya ukodishwaji wa boti hizo, hali hii imepelekea Wizara kuchukuwa hatua ya kuzirudisha boti hizo chini ya ZAFICO. Aidha, katika kuendeleza azma ya ukodishwaji wa boti hizo, Kampuni ya ZAFICO iliingia makubaliano ya ukodishwaji wa boti hizo na Kampuni ya "Muyuni Fishing and logistics Limited" ambapo tayari imefanya malipo ya awali ya miezi 3 wa meli zote mbili za Sehewa. Hivi sasa meli

hizo zimeanza kazi pamoja na kuelimisha vijana 6 wa Kizanzibari ili kupata uzowefu wa Uvuvi wa Bahari Kuu.

ix. Vile vile, Kampuni ya ZAFICO iliingia mkataba na Kampuni ya Indepth Limited kwa ajili ya ujengaji na ufungaji wa chanja 2,210 za kuanikia dagaa zenye thamani ya **Shilingi 1,989,000,000** ambapo jumla ya chanja 1,200 tayari zimekamilika. Kukamilika kwa ujenzi wa chanja hizo kunategemea na kuanza kwa ujenzi wa Kiwanda cha KAMA na Ndagoni.

**47. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Kampuni ya Uvuvi ZAFICO iliombewa jumla ya **Shilingi 964,846,172.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 428,100,000** ni Ruzuku ya Mishahara kutoka SMZ na **Shilingi 536,746,172** kwa utekelezaji wa Mradi wa uwekaji wa mitambo ya kuhifadhia baridi (KOICA). Hadi kufikia Machi 2024, Kampuni imepatiwa jumla ya **Shilingi 293,403,726** sawa na asilimia **30.41** ya fedha zilizopangwa.

**MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU – DSFA**

**48. Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Mamlaka imetoa leseni za uvuvi wa bahari kuu 67 kwa meli moja (1) ya ndani na 56 za nje, na vibali vine (4) vya kuvua nje ya mipaka ya Tanzania (Areas beyond national jurisdiction) na leseni sita (6) kwa meli saidizi (supply vessel) na kukusanya jumla ya **Shilingi 9,700,000,000,** ikilinganishwa na leseni 51 zilizotolewa na kukusanya jumla ya **Shilingi 6,800,000,000** kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Kuimarika kwa makusanyo yatokanayo na leseni za uvuvi wa bahari kuu kunatokana na juhudi za makusudi zinazoendelea kufanywa na DSFA ikiwa ni pamoja na kufanya mazungumzo na wamiliki wa meli

na kuwepo kwa mazingira rafiki ya kuvutia uwekezaji yaliyopo sasa kutokana na utekelezaji wa Sheria ya Uendelezaji na Usimamizi wa Uvuvi wa Bahari Kuu Sura 388 ya mwaka 2020 na Kanuni zake za mwaka 2021.

ii. Mamlaka inaendelea kuimarisha ufuatiliaji, udhibiti na uangalizi (Monitoring, Control and Surveillance - MCS) kwenye bahari kuu kwa kutumia mifumo yake ya kufuatilia mienendo ya meli (Vessel Monitoring System - VMS na Automatic Identification System – AIS), kukagua meli kabla ya kutoa leseni za uvuvi, kufanya doria ya kwenye maji yetu kupitia doria ya kikanda iliyofanyika Machi - Aprili 2024, kuweka Waangalizi wa Uvuvi kwenye meli zilizochukua leseni na kubadilishana taarifa na nchi jirani na taasisi za kikanda.

iii. Katika kupunguza upotevu wa mazao ya samaki baada ya kuvuliwa (post-harvest losses) na kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi kwa wavuvi wadogo, ALBACORA Group imetoa mtambo wa kuzalisha barafu uliosimikwa katika soko la samaki la Malindi – Unguja wenye uwezo wa kuzalisha tani tano (5) za barafu kwa siku. Mtambo wa pili utasimikwa Dar es Salaam ndani ya robo ya kwanza ya mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, katika mwaka 2023/2024 ALBACORA Group imeshusha tani 25 za samaki wasiolengwa katika bandari ya Malindi Zanzibar pamoja na kutoa mafunzo ya vitendo na ajira kwa mabaharia sita (6) wa Kitanzania (Tanzania bara - 3 na Zanzibar - 3)

## PROGRAMU NDOGO YA UHIFADHI WA MAENEO YA BAHARI

**49. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kutoa elimu ya Uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii na kuzijengea uwezo kamati za uvuvi 102 Unguja

na Pemba ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi na kusimamia rasilimali za bahari kwa kuanzisha maeneo ya ufungaji wa pweza na samaki wa miambani.

ii. Kwa kushirikiana na Shirika la Maendeleo la UNDP Idara imeendelea na kusimamia uanzishwaji wa mifumo ya kieletroniki ya ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya hifadhi.

iii. Kamati 7 za uongozi shirikishi (Community Management Groups) ziliundwa na kupatiwa mafunzo juu ya usimamizi wa rasilimali za baharini. Aidha vikao 3 na taasisi zisizo za Serikali na wadau wa utalii kuhusu uhifadhi wa mazingira na kufanya utalii endelevu vilifanyika.

iv. Idara imeanza kutumia mifumo ya ZanMalipo katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo ya hifadhi.

v. Doria shirikishi 220 zilifanyika katika maeneo yote ya hifadhi za bahari kwa lengo la kudhibiti uvuvi haramu (Nyavu za macho madogo, bunduki na madema ya waya na matumizi ya gesi pamoja na kutia nanga katika matumbawe).

vi. Vyombo 47 vilikamatwa vikivua uvuvi usiokubalika katika hifadhi za bahari. Ambapo kesi zao zilihukumiwa nje ya mahkama kwa kupewa elimu ya uhifadhi na wengine kulipa faini ya **Shilingi 1,350,000.**

vii. Aidha boti mbili za doria zilikabidhiwa kwa kamati shirikishi za hifadhi ya MENAI na TUMCA. Boti hizo zimefadhiliwa na Taasisi ya MCCC LTD kwa ajili ya kufanya doria za kudhibiti uvuvi haramu.

viii. Maeneo 2 yamewekewa matumbawe bandia, Maeneo 4 ya ufungaji wa miamba ya Pweza na samaki wa miambani yamefunguliwa na maeneo 8 tengefu ya miamba yamedhibitiwa kwa kuruhusu matumizi ya mitego

maalumu tu, ili kuimarisha afya ya bahari. Maeneo hayo ni Uroa, Michamvi, Ukongoroni, Marumbi, Mtende, Fundo, Gando na Kukuu na maeneo mawili ya Mnemba na Jambiani yamewekwa matumbawe bandia na kazi ya ufuatiliaji inaendelea.

ix. Taratibu za kuanzisha maeneo mawili mapya ya hifadhi katika Kisiwa cha Pemba zinaandaliwa. Aidha wafanyakazi 5 walishiriki mafunzo ya muda mfupi kuhusu kuimarisha mawasiliano na mashirikianon ya Kimaeneo na Kikanda katika usimamizi wa rasiliamali za bahari. Mafunzo hayo yalifanyika Kunduchi na yalifadhiliwa na WIOMSA.

x. Idara imekuwa ikishirikiana na wadau mbali mbali wa kimaendeleo ili kuendeleza kazi za uhifadhi, wadau hao ni; UNDP, USAID heshimu baharí, MCCC LTD, Blue Ventures pamoja na WCS.

50. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Programu hii ndogo ya Uhifadhi imeombewa jumla ya **Shilingi 3,958,736,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 343,336,000** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 3,615,400,000** ni kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024, Programu imepatiwa Jumla ya **Shilingi 85,378,644** sawa na asilimia **2.16** ya fedha iliyopangwa.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ufanisi na ustawi wa sekta.

**Programu imegawika katika programu ndogo tatu nazo ni:**

i. Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji

ii. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti

iii. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba.

52. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeombewa jumla ya **Shilingi 6,399,787,300** kati ya fedha hizo **Shilingi 2,899,787,300** ni kwa Matumizi ya Kawaida ambapo **Shilingi 1,760,683,300** ni Mishahara, **Shilingi 1,139,104,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 3,500,000,000** ni kwa kutekeleza miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Machi 2024, Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi 1,932,878,594** sawa na asilimia **30.20.** kati ya fedha hizo **Shilingi 1,481,672,808** ni Mishahara, **Shilingi 451,205,786** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**PROGRAMU NDOGO YA UTUMISHI NA UENDESHAJI.**

53. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

54. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024 programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Jumla ya Wafanyakazi 221 wamepatiwa stahiki zao.

ii. Jumla ya wafanyakazi 60 wamepatiwa mafunzo; wafanyakazi (8) wamepatiwa mafunzo ya muda mrefu na hamsini na mbili (52) mafunzo ya muda mfupi.

iii. Jumla ya wafanyakazi 46 wamepatiwa mikataba ya kupima majukumu yao ya kazi.

iv. Hatua za udhibiti wa mali za Serikali ziliendelea kuchukuliwa kwa mujibu wa taratibu zilizopangwa na kuwasilishwa Ofisi ya Msajili wa Hazina. Mali hizo chakavu zinajumuisha samani za ofisini na vifaa vya TEHAMA.

v. Kukamilisha Kanzidata ya rasilimali watu (Human Resource Database) na kukamilika kwa Tovuti ya Kiswahili chini ya ufadhili wa WIOMSA na hatua za kutengeneza ya Kiingereza inaendelea kwa mwaka wa fedha ujao.

vi. Kazi ya utengenezaji wa Mkataba wa huduma umekamilika na upo katika hatua ya kupelekwa kwa Wadau.

vii. Kuendelea kuimarisha utoaji wa taarifa za Wizara kwa jamii ambapo machapisho 71 kupitia mtandao wa facebook, Twitter na Instagram na vipindi 60 vya TV na redio vimetolewa.

55. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024 Programu ndogo ya Utawala na Uendeshaji, imeombewa jumla ya **Shilingi 1,430,039,380** kwa kazi za kawaida, kati ya fedha hizo **Shilingi 829,843,380** ni Mishahara na **Shilingi 600,196,000** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2024 Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi 1,066,476,514** sawa na asilimia **74.58.** kwa kazi za kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 738,861,970** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 327,614,544** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

56. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Programu ndogo hii inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kushirikiana na Wizara ya Mifugo na Uvuvi (SMT) katika kusajili na hatimae kuruhusu usafirishaji wa mwani na mazao mengine ya baharini kutoka Zanzibar moja kwa

moja kwenda katika soko la China ambapo hadi sasa makampuni 12 yamesajiliwa.

ii. Kuwasilishwa Sheria tatu (3) za Wizara (Sheria ya Uvuvi, Uhifadhi wa Bahari na Utafiti wa Maliasili za Bahari katika vikao vya Baraza la Mapinduzi. Sheria hizo zishawasilishwa Kamati ya Sheria na Katiba ya Baraza la Mapinduzi na Sheria ya ZAFIRI imeshapitishwa na Baraza la Wawakilishi.

iii. Kushirikiana na Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali katika ukusanyaji wa Takwimu za ajira zilizozalishwa kuanzia Novemba 2020 hadi Oktoba 2023 katika sekta ya Uchumi wa Buluu ili kutathmini utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi Ibara ya 13 (b) la kuzalisha ajira 300,000 ifikapo 2025.

iv. Kuwasilisha Ripoti ya mwaka ya Takwimu za sekta ya uvuvi kwa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

v. Kushiriki katika mchakato wa Tanzania wa kuripoti utekelezaji wa Mkataba wa Kimataifa wa Haki za binadamu.

vi. Kushiriki katika vikao vya Tume za Pamoja za Ushirikiano (JPC) na nchi mbali mbali. Kushiriki katika kikao cha mashirikiano kati ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Tanzania Bara na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

vii. Kushirikiana na Tume ya Mipango Zanzibar katika kufuatilia utekelezaji wa kazi za kawaida na Miradi ya Maendeleo na kuziwasilisha katika Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi.

57. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti kwa mwaka 2023/2024 imeombewa jumla ya **Shilingi 3,872,045,660.** Kati ya Fedha hizo **Shilingi 112,045,660** ni Mishahara, na **Shilingi 260,000,000** ni Matumizi ya

Uendeshaji wa Ofisi. Katika kutekeleza Mradi wa Jumuishi wa kuhifadhi ikolojia na kuendeleza uchumi wa bahari, programu hii imeombewa jumla ya **Shilingi 3,500,000,000.** Hadi kufika Machi 2024, Proramu imepatiwa jumla ya **Shilingi 185,767,602** sawa na asilimia **4.80**. Kati ya Fedha hizo **Shilingi 116,260,950** ni Mishahara, na **Shilingi 96,506,652** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI PEMBA.**

58. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu utekelezaji wa kazi za mipango ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa upande wa Pemba.

59. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024, Programu hii imetekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu ziara saba (7) za viongozi wa Wizara na Kitaifa.

ii. Kushiriki katika maadhimisho mbali mbali ya kitaifa ikiwemo maadhimisho ya siku ya wanawake duniani.

iii. Kufuatillia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, na taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba.

iv. Vikao vinne (4) vimefanyika ikiwemo kujadili mapato yatokanayo na eneno la hifadhi ya bahari Pemba (PECCA), kujadili changamoto za uvuvi na mwani kwa pamoja na wajumbe wa kamati za Uvuvi na Mwani za Wete, kujadili maendeleo ya hifadhi na maendeleo ya jamii kwa pamoja na kamati tendaji ya PECCA na kikao cha kupitia modeli ya mkataba wa mgawanyo wa mapato ya uzalishaji wa Mafuta na Gesi asilia.

v. Kufanyika kwa vikao mbali mbali vya uendeshaji na usimamizi wa Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana na Idara na taasisi mbali mbali mtambuka za Sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba.

vi. Kufuatilia utekelezaji wa kazi za Wizara maofisini, na taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi - Pemba.

**60. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba, kwa Mwaka wa Fedha wa 2023/2024, Programu hii imeombewa jumla ya **Shilingi 1,097,702,260** ni kwa Matumizi ya Kawaida , Kati ya fedha hizo **Shilingi 818,794,260** ni Mishahara na **Shilingi 278,908,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Hadi kufikia Machi 2023, Programu imepatiwa jumla ya **Shilingi 680,634,478** sawa na asilimia **62.01** Kati ya fedha hizo **Shilingi 54,084,590** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 626,549,888** ni Mishahara.

## CHANGAMOTO

**61. Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitahada za Wizara na Serikali kwa ujumla, Baadhi ya changamoto zilizojitokeza katika kutekeleza malengo yaliyowekwa ni pamoja na :

| Nam | Changamoto | Hatua zilizochukuliwa |
|---|---|---|
| 1 | Upungufu wa watendaji. | Wizara imewasilisha Serikalini ombi la wafanyakazi wapya na tayari wameanza kuajiriwa Pemba (35) na Unguja (23). |
| 2 | Uhaba wa teknolojia na nyenzo za kufanyia kazi. | Wizara ilipatiwa vifaa vya Afisi kutoka SMZ na UNDP. Wizara pia imeomba gari saba Serikalini ambapo bado hazijapatikana. |
| 3 | Kuwepo matukio ya Uvuvi Haramu. | Elimu na doria zinafanyika pamoja na kuweka misingi mipya ya Sera na Sheria za Sekta ya Uvuvi. |
| 4 | Uhaba wa Wataalamu wa Uvuvi wa Bahari Kuu kwa Kampuni ya ZAFICO. | Wizara inaendelea na utaratibu wa kuwajengea uwezo na uzoefu wazawa kuweza kushiriki katika uvuvi wa kibiashara wa bahari kuu kwa kutumia njia mbali mbali ikiwemo kuwapatia kazi katika meli za uvuvi wa bahari kuu zenye makubaliano na Serikali kama vile meli zinazomilikiwa na Kampuni ya Albacora. Hadi sasa jumla ya vijana wa kizanzibar 12 wamepata mafunzo na uzoefu katika meli inayovua katika ukanda wa Magharibi ya Bahari ya Hindi. |

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA BAJETI INAYOZINGATIA PROGRAMU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

### MAKADIRIO YA MAPATO 2024/2025

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha wa 2024/2025, Wizara imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 5,921,700,000** kutoka vianzio vyake 5 vya Unguja na Pemba (**Kiambatisho Namb. 6**).

### MAKADIRIO YA MATUMIZI 2024/2025

63. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi 66,012,766,000** kwa ajili ya Kazi za Kawaida na Miradi ya Maendeleo ya Wizara. Kati ya fedha hizo **Shilingi 10,985,000,000** ni kwa Kazi za Kawaida na **Shilingi 55,027,766,000** ni kwa Kazi za Maendeleo. (**Kiambatisho Namb. 7**).

64. **Mheshimiwa Spika,** mgawanyiko wa fedha za kawaida ni **Shilingi 10,985,000,000.** Kati ya hizo, **Shilingi 4,130,200,000** ni Mishahara, **Shilingi 2,501,400,000** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 4,353,400,000** ni Ruzuku kutoka SMZ. Kwa fedha za Ruzuku, **Shilingi 1,177,700,000** ni kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar, **Shilingi 2,788,900,000** ni kwa ajili ya Mamlaka ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia, na **Shilingi 386,800,000** ni kwa ajili ya Kampuni ya ZAFICO.

65. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi 55,027,766,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo,**.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 39,000,000,000** ni kutoka SMZ na **Shilingi 16,027,766,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo, ambapo **Shilingi 13,346,994,000** ni Mkopo na **Shilingi 2,796,172,000** ni Ruzuku (**Kiambatisho**

**Namb. 8**). Aidha, jumla ya **Shilingi 4,500,000,000** zimetengwa kupitia bajeti ya Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ajili ya matumizi ya Kazi za Kawaida kwa Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC).

## UTEKELEZAJI WA PROGRAMU ZA WIZARA

**66. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 itatekeleza malengo yake kupitia Programu zake kuu tatu ambazo ni:

i. Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu;

ii. Programu ya Maendeleo ya Uvuvi;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

## UTEKELEZAJI WA MIRADI YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025

**67. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara imepanga kutekeleza Miradi ya Maendeleo nane (8) yenye thamani ya **Shilingi 55,027,766,000:**

i. Mradi wa kuendeleza Kilimo na Uvuvi unaofadhiliwa na Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (AFDP-IFAD);

ii. Mradi wa Kuanzisha Kituo cha Kuhifadhia Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (SMZ);

iii. Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Bidhaa za Petroli iliyosafishwa na Usambazaji (SMZ);

iv. Ujenzi wa Diko na Soko la kisasa (SMZ);

v. Mradi wa kuboresha miundombinu ya Maabara ya Uthamini wa Ubora wa Bidhaa za baharini (SMZ);

vi. Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini unaofadhiliwa na Shirika la KOICA.

vii. Mradi wa Utafiti wenye lengo la Kudumisha Uchumi, Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii unaofadhiliwa na Shirika la NORAD.

viii. Mradi wa Tathmini ya Ubora wa Maji ya Bahari unaofadhiliwa na Shirika la UNEP.

**68. Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia Kampuni ya Uvuvi Zanzibar– ZAFICO imepanga kuendelea kutekeleza miradi ya ubia na makampuni ya ndani na nje ya nchi kama ifuatavyo;

i. Mradi wa uwekaji wa Mitambo ya Kuhifadhi Baridi (Pilot Implementation and Development of Zero Energy Seafood chain) unaofadhiliwa na Shirika la KOICA.

ii. Mradi wa ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa Ndagoni.

iii. Kuendelea na Ujenzi wa Kiwanda cha kusarifu dagaa katika eneo la Kama kupitia ufadhili wa Serikali na mikopo ya Benki.

**69. Mheshimiwa Spika,** aidha; Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa mwaka wa fedha 2024/2025 itatekeleza jumla ya miradi mengine mitano (5) kwa mashirikiano na Taasisi zisizo za Serikali (NGO's) kama ifuatavyo;

i. Mradi wa Heshimu Bahari unaofadhiliwa na USAID wenye thamani ya Dola za Kimarekani US$ Milioni 13,000,000.

ii. Mradi wa Bahari Mali unaofadhiliwa na Ubalozi wa Jamhuri ya Ireland wenye thamani ya Euro Milioni 1,800,000.

iii. Mradi wa Bahari ni Urithi unaotekelezwa na Shirika la WCS kupitia mfuko wa "Blue Action Fund" wenye thamani ya Euro Milioni 5,800,000.

iv. Mradi wa Usimamizi wa Kijamii wa Maeneo ya Kiikolojia ya Bahari unaotekelezwa na Shirika la Mwambao kupitia "Blue Action Fund". Mradi huu unagharimu Euro Milioni 6,400,000.

v. Mradi wa Miamba Yetu unaofadhiliwa na "Global Fund for Coral Reefs" wenye thamani ya US$ Milioni 2,000,000.

**70. Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi itaendelea na uwezeshaji wa jamii kwenye miradi ya kuleta Ahueni ya UVIKO 19. Aidha, pamoja na miradi hiyo, Wizara itashajihisha jamii kupitia Programu ya uwezeshaji ya wadau wa sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi "Blue Economy Intervention Plan".

## MALENGO YA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI KWA MWAKA 2024/2025

**71. Mheshimiwa Spika,** lengo kuu la Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi ni Kukuza Uchumi wa Zanzibar kwa kuimarisha matumizi endelevu ya bahari pamoja na kuwawezesha wajasiriamali ili kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana za kisasa, mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya uwekezaji na uimarishaji wa minyororo ya thamani (miundombinu na huduma) ambayo itasaidia upatikanaji wa ajira na masoko kwa vijana kupitia Uchumi wa Buluu.

**72. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi inatarajia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo;

i. Utoaji wa elimu na uelewa katika masuala ya Uchumi wa Buluu ikiwemo mbinu, nyenzo, mitaji na utafutaji wa masoko kwa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla.

ii. Uwezeshaji na Uwekezaji katika Uvuvi Endelevu wa Mwambao na Bahari Kuu.

iii. Uwezeshaji na Uwekezaji katika Kilimo cha Mwani.

iv. Uwezeshaji na Uwekezaji katika Ufugaji wa Viumbe Maji kama vile Majongoo Bahari, Kaa na Samaki.

v. Utafiti na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na Nishati Mbadala za Baharini

vi. Ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi pamoja na biashara ya Mafuta na Gesi

vii. Ujenzi wa Miundo Mbinu ya Bandari za uvuvi, Madiko, Masoko, Viwanda, Huduma na Biashara za Mazao ya Baharini.

viii. Utafiti wa Uvuvi, Sayansi za Bahari, Maliasili za Bahari, Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi Baharini

ix. Uhifadhi wa Maeneo ya Bahari (Matumbawe, Nyasi Bahari, Mikoko na Bioanuwai ya Baharini).

x. Utalii Endelevu wa Mwambao na Bahari.

xi. Usimamizi wa Bahari (Usalama wa Bahari, Kuimarisha Ulinzi wa Bahari na Kupambana na Uvuvi Haramu Usioripotiwa).

xii. Kuweka misingi imara na kuimarisha utekelezaji wa bajeti inayozingatia jinsia na watu wenye mahitaji maalumu (**Kiambatisho Nam.9**).

**73. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi imeweka malengo ya usimamizi endelevu wa Bahari katika kuimarisha Maendeleo ya Uchumi wa Buluu Zanzibar kama ifuatavyo;

i. Kusimamia Maendeleo Endelevu ya Sekta ya Uvuvi, Mwani na Mazao ya Baharini.

ii. Kusaidia na kushajihisha fursa mbali mbali za uwekezaji na ubia baina ya Sekta za Umma na Sekta Binafsi katika Uchumi wa Buluu.

iii. Kutekeleza malengo ya uwezeshaji wa wajasiriamali na wananchi kwa ujumla katika Uchumi wa Buluu.

iv. Kusimamia Utafutaji na Uchimbaji wa Rasilmali ya Mafuta na Gesi Asilia pamoja na uwekezaji katika biashara ya Mafuta na Gesi Asilia.

v. Kuendelea na juhudi za utafiti na uwezo katika kutafuta fursa mbali mbali za nishati mbadala.

vi. Kupambana na uharibifu na uchafuzi wa mazingira ya bahari na kusimamia hifadhi za maeneo ya bahari.

vii. Kusimamia na kuendeleza Tafiti za Sekta ya Uvuvi na Rasimali za Bahari.

viii. Kuongeza mashirikiano na Sekta mbali mbali katika uratibu wa masuala ya diplomasia ya Uchumi wa Buluu, usimamizi na usalama wa Bahari.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU

**74. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu imegawika katika Programu ndogo moja nayo ni Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu. Aidha, Programu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu ina huduma zake kuu mbili ambazo;

i. Uratibu wa Uchumi wa Buluu

ii. Udhibiti wa Ufuatiliaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar.

75. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya jumla ya **Shilingi 11,205,996,000** kwa ajili ya Programu Kuu ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu**.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 417,096,000** kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, **Shilingi 2,788,900,000** ni Ruzuku kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uendelezaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) na **Shilingi 8,000,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo.

**PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UCHUMI WA BULUU**

76. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu inalenga kuratibu na kutekeleza masuala mtambuka yanayohusiana na Uchumi wa Buluu kwa ujumla. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu ndogo ya Uchumi wa Buluu kupitia huduma zake inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendeleza, kuwezesha, kutekeleza, kufuatilia na kuratibu MSP- Zanzibar;

ii. Kuratibu sekta za kipaumbele za Uchumi wa Buluu;

iii. Kuhamasisha na kujenga uwezo kwa jamii kuhusu Uchumi wa Buluu;

iv. Kuratibu Masuala ya Uwezeshaji na Uongezaji wa Thamani wa Mazao ya Baharini na upatikanaji wa Masoko;

v. Kuratibu ushiriki wa kitaifa, kikanda na Kimataifa katika shughuli za Uchumi wa Buluu; na

vi. Kuratibu utambuzi wa mahitaji ya kuandaa na kusimamia “Dashboard” ya Uchumi wa Buluu na “Satellite Account”.

77. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha Matumizi ya Jumla ya **Shilingi 417,096,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Maendeleo ya Uchumi wa Buluu.

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA UTAFUTAJI NA UCHIMBAJI WA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR (ZPRA).**

78. **Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) inalenga kuendeleza majukumu yake ya kusimamia na kudhibiti shughuli zote za utafutaji na uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia hapa Zanzibar.

79. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia imepanga kutekeleza Majukumu yake kupitia vipaumbele vifuatavyo;

i. Kuendelea na zoezi la kuvitangaza vitalu vinane (8) vipya vilivyopo Mashariki mwa bahari ya Zanzibar kupitia majukwaa mbali mbali ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa pamoja na kukaribisha wawekezaji kwa ajili ya shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kusimamia utekelezaji wake.

ii. Kuendelea na programu ya ugawaji upya wa vitalu kwa eneo la kitalu cha Pemba – Zanzibar pamoja na kuvitafutia wawekezaji kwa ajili ya shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia na kusimamia utekelezaji wake.

iii. Kukamilisha majukumu ya kisheria na kimkataba ikiwemo ulipaji wa fidia kwa wananchi waliobakia kutokana na zoezi la Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia kwa njia ya mtetemo lililofanywa na kampuni ya RAKGas.

iv. Kukamilisha miundombinu kwa ajili ya matumi ya kituo cha muda cha uhifadhi wa Taarifa (Temporary Data Center) kupitia mradi wa NDR pamoja na kutoa taarifa na machapisho kuhusiana na shughuli za Utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia nchini.

v. Kuendeleza mashirikiano na wadau mbali mbali wa sekta wa ndani na nje wakiwemo washirika wa maendeleo kwa ajili ya usimamizi endelevu wa shughuli za Mafuta na Gesi Asilia nchini.

vi. Kuimarisha mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano – TEHAMA ndani ya Mamlaka ili kuwezesha muingiliano wa karibu ya kiutendaji baina ya Idara, Vitengo na Divisheni zake.

vii. Kuendesha Programu za kukuza uelewa kwa wananchi kuhusiana na masuala ya Mafuta na Gesi Asilia ambapo jumla ya program 54 zimepangwa kuanyika kupitia mikutano ya hadhara katika shehia, mikutano ya Taasisi, makongamano pamoja na vyombo vya Habari.

viii. Kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa Mamlaka ikiwemo ubora wa ofisi, nguvu kazi na maslahi ya watendaji pamoja na kuwajengea uwezo waliopo ili kuchochea uwajibikaji wao na kuongeza ufanisi.

80. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 6,788,900,000** kwa ajili ya Mamlaka ya Udhibiti wa Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPRA) Kati ya Fedha hizo **Shilingi 1,864,900,000** ni Mishahara, **Shilingi 924,000,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi na **Shilingi 4,000,000,000** ni kwa utekelezaji wa Mradi wa NDR.

**KAMPUNI YA MAENDELEO YA MAFUTA NA GESI ASILIA ZANZIBAR, ZPDC**

81. **Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar inalenga kuendeleza utafutaji wa Mafuta na Gesi Asilia pamoja na kuwajengea uwezo watendaji wa kampuni. Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Ujenzi wa Bohari ya kuhifadhia mafuta yenye ujazo wa MT 50,000.

ii. Kujenga mazingira bora ya kufanyia kazi kwa Wafanyakazi.

iii. Kujenga uwezo kwa Watendaji wa Kampuni katika Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia.

iv. Kushiriki katika shughuli za mkondo wa juu wa mafuta na gesi Zanzibar.

v. Kutoa uelewa wa Sekta ya Mafuta na Gesi Asilia kwa Taasisi za Serikali na wananchi.

82. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 6,000,000,000** kwa ajili ya Kampuni ya Maendeleo ya Mafuta na Gesi Asilia Zanzibar (ZPDC). Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya uendeshaji wa Kampuni na **Shilingi 4,000,000,000** kwa kutekeleza Mradi wa ujenzi wa kituo cha kuhifadhia bidhaa za petroli iliyosafishwa.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA UVUVI

83. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Maendeleo ya Uvuvi imegawika katika Programu ndogo mbili ambazo ni Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi na Ufugaji wa Mazao ya Baharini na Programu ndogo ya Uhifadhi wa Maliasili za Bahari.

84. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 51,089,282,000** kwa ajili ya Programu Kuu ya Maendeleo ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo **Shilingi 4,061,516,000** ni kwa Matumizi ya Kawaida ambapo, **Shilingi 1,744,212,000** ni Mishahara, **Shilingi 752,804,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi, na **Shilingi 1,564,500,000** ni Ruzuku. Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo Programu hii inaombewa

jumla ya **Shilingi 47,027,766,000.** Kati ya hizo **Shilingi 31,000,000,0000** kutoka SMZ na **Shilingi 16,027,766,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

## PROGRAMU NDOGO YA MAENDELEO YA UVUVI NA UFUGAJI WA MAZAO YA BAHARINI

**85. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi dhumuni lake kubwa ni kuendeleza Uvuvi na kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao mengine ya baharini kwa njia ya ufugaji. Programu ndogo hii kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuimarisha kilimo cha mwani na kuongeza uzalishaji wa mwani kutoka tani 16,564 hadi tani 20,000 kwa kuwapatia wakulima elimu na vifaa vya kisasa vya kilimo.

ii. Kutoa elimu ya juu ya Uvuvi bora na endelevu kwa wavuvi wadogowadogo.

iii. Kutoa elimu ya ufugaji wa mazao ya baharini kwa wafugaji.

iv. Ujenzi wa masoko na madiko mawili ya kisasa Unguja na Pemba kwa lengo la kuimarisha sekta ya Uvuvi.

v. Kuimarisha usarifu wa mazao ya baharini kwa kujenga vituo vya usarifu na uongezaji wa thamani wa mazao ya baharini ikiwemo mwani Unguja na Pemba.

vi. Kuimarisha usimamizi na uratibu wa idara ya maendeleo ya uvuvi na mazao ya baharini ili kuongeza ufanisi katika kutekeleza shughuli za sekta ya maendeleo ya uvuvi na mazao ya baharini.

vii. Kutengeneza kanuni na miongozo katika kuimarisha uvuvi na ufugaji wa mazao ya baharini.

86. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 50,745,946,000.** kwa ajili ya Programu ndogo ya Maendeleo ya Uvuvi. Kati ya fedha hizo **Shilingi 3,718,180,000** kwa Matumizi ya Kawaida, ambapo Shilingi 1,744,212,000 ni Mishahara, **Shilingi 409,468,000** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji ya Ofisi na **Shilingi 1,564,500,000** ni Ruzuku kwa ajili ya ZAFIRI na ZAFICO. Katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo, Programu hii inaombewa jumla ya **Shilingi 47,027,766,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 31,000,000,000** kutoka SMZ na **Shilingi 16,027,766,000** ni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

**TAASISI YA UTAFITI WA UVUVI NA MALIASILI ZA BAHARINI ZANZIBAR (ZAFIRI)**

87. **Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuendeleza tafiti za kuimarisha Sekta ya Uvuvi.
ii. Kuimarisha miundombinu ya maabara ya microbiolojia na kemia.
iii. Usambazaji wa matokeo ya utafiti wa Uvuvi.
iv. Kukuza mashirikiano na Taasisi nyengine za ndani na nje ya nchi
v. Kuandaa kanuni zinazohusiana na Sheria ya kuundwa kwa Taasisi ya ZAFIRI, Sheria nambari 11 ya mwaka 2023.
vi. Kuimarisha usimamizi na uendeshaji wa Taasisi ya ZAFIRI
vii. Kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi wa Taasisi.

88. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 5,458,472,000** kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Baharini Zanzibar (ZAFIRI). Kati ya Fedha hizo **Shilingi 1,177,700,000**

ni Rukuzu kutoka SMZ ambapo **Shilingi 889,700,000** ni Mishahara na **Shilingi 288,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi. Aidha, **Shilingi 4,280,772,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za Maendeleo ambapo **Shilingi 4,000,000,000** kwa utekelezaji wa Mradi wa kuboresha miundombinu ya maabara ya uthamini wa ubora wa mazao ya baharini, na **Shilingi 280,772,000** kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (**Shilingi 41,072,167** kwa kutekeleza Mradi wa utafiti wenye lengo la kudumisha uchumi, usalama wa chakula na maisha endelevu kwa jamii (Mradi Samaki), na **Shilingi 239,700,000** kwa utekelezaji wa mradi wa tathmini ya ubora wa maji ya bahari.

**KAMPUNI YA UVUVI ZANZIBAR – ZAFICO**

**89. Mheshimiwa Spika,** Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

i. Kuendelea na utaratibu wa ununuzi wa meli ya uvuvi kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi - IFAD.

ii. ZAFICO kupitia Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi (IFAD) inaendelea na mchakato wa Ujenzi wa Kiwanda Jumuishi cha kuchakata samaki na mitambo ya baridi kitakachojengwa Fungurefu- Mkokotoni.

iii. Kuimarisha mifumo ya baridi na uhifadhi wa samaki na mazao ya baharini.

iv. Kushirikiana na sekta binafsi katika kuendeleza uvuvi na ufugaji wa kisasa wa mazao ya baharini (samaki, Kamba) kupitia Shirika la KOICA.

v. Kuwawezesha wajasiriamali kuongeza thamani na ubora wa dagaa wa Zanzibar.

vi. Kuendeleza Mradi wa Uuzaji wa Samaki.

vii. Kukamilisha ujenzi wa kituo cha kusarifu dagaa Ndagoni - Pemba

viii. Kuendeleza utekelezaji wa Mradi wa samaki wa matenga wa Kampuni ya Zanzibar Aquaculture Harvest Company (ZAHC).

**90. Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 386,800,000** kwa ajili ya Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) ambayo ni Ruzuku ya Mishahara kutoka SMZ.

**MAMLAKA YA KUSIMAMIA UVUVI WA BAHARI KUU -DSFA**

**91. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kutoa leseni 71 za Uvuvi kwa meli za Uvuvi wa Bahari Kuu kutoka ndani na nje ya nchi ambapo kiasi cha **Shilingi bilioni 10.8** zitakusanywa kutokana na leseni na vibali vya Uvuvi, na kuuza bycatch.

ii. Kushirikiana na kampuni ya ALBACORA itatekeleza mpango wa ujenzi wa kiwanda cha kuchakata samaki katika Manispaa ya Tanga.

iii. Kuendelea kutoa elimu kwa wadau kuhusu vivutio na fursa zinazopatikana kwenye Uvuvi wa Bahari Kuu na kuimarisha utekelezaji wa Sheria na Kanuni za Usimamizi na Uendelezaji wa Uvuvi wa Bahari Kuu, na kufanya mazungumzo na wawekezaji zaidi wa ndani na nje ya nchi ili kuchukua leseni za Uvuvi wa Bahari Kuu na kuweka katika miundombinu muhimu.

iv. Kuimarisha ulinzi na usalama wa rasilimali za Uvuvi katika ukanda wa uchumi wa bahari kwa kuweka Waangalizi wa Uvuvi na kufanya ukaguzi wa meli zitakazoomba leseni na zitakazokuwa zikivua kwa

kufanya doria za anga na kwenye maji kwa kushirikiana na jumuiya za kikanda.

v. Kuendelea kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa utafiti na kuwezesha upatikanaji wa taarifa kuhusu maeneo yenye samaki wengi (Potential Fishing Zones - PFZ) baharini kwa kutumia simu janja

**PROGRAMU NDOGO YA UHIFADHI WA MALIASILI ZA BAHARI**

**92. Mheshimiwa Spika,** kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kutoa elimu ya Uhifadhi wa mazingira ya bahari kwa jamii na kuzijengea uwezo kamati shirikishi za uvuvi Unguja na Pemba ili kuongeza ufanisi katika shughuli zao za uvuvi na kusimamia rasilimali za bahari katika maeneo ya uhifadhi.

ii. Kuanzisha mfumo wa ufuatiliaji kwa viumbe walio hatarini kutoweka ili kuimarisha uhifadhi wa viumbe hao.

iii. Kuanzisha kanuni na miongozo ya usimamizi wa wanyama wa bahari ikiwemo pomboo na viumbe wengine katika maeneo ya hifadhi.

iv. Kuimarisha Doria /Ulinzi shirikishi 340 katika maeneo ya Maji ya Ndani kwa kununua Boti 3 za Doria ili kudhibiti Uvuvi haramu.

v. Kuongeza maeneo mapya mawili ya hifadhi Pemba-Kusini Mashariki na Kaskazini Mashariki.

vi. Kufanya ufuatiliaji katika maeneo ya miamba na mazalia ya samaki, kuwawezesha jamii kuweka matumbawe bandia na kufanya usafi wa matumbawe katika maeneo ya Hifadhi za bahari ili kuongeza uzalishaji wa samaki.

vii. Kuimarisha mazingira bora katika maeneo ya hifadhi.

viii. Kuwapatia mafunzo wafanyakazi kumi kuhusu usimamizi wa uhifadhi wa mazingira ya bahari.

ix. Kutengeneza kanuni za maeneo ya hifadhi za bahari na kuanzisha sheria ndogo ndogo za usimamizi wa rasilimali za uvuvi katika vijiji vilivyomo pembezoni mwa bahari

x. Kushirikiana na washirika wa kimaendeleo katika kuendeleza uhifadhi wa mazingira ya baharini.

93. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 343,336,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Uhifadhi.

## PROGRAMU KUU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI

94. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi lengo lake kubwa ni kutoa huduma za kiofisi kwa ustawi na ufanisi wa sekta. Programu imegawika katika programuu ndogo tatu nazo ni:

i. Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji

ii. Programu ndogo ya Mipango Sera na Utafiti

iii. Programu ndogo ya Uratibu wa kazi za Uchumi wa Buluu Afisi kuu Pemba

95. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 3,717,488,000** kwa ajili ya Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi**.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 2,385,988,000** kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,331,500,000** kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU NDOGO YA UTUMISHI NA UENDESHAJI

96. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji ina lengo la kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi kwa ufanisi na maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

    i. Kuimarisha mazingira bora ya utendaji kazi na miundombinu ya mawasiliano.

    ii. Kufuatilia na kudhibiti Mali za Serikali

    iii. Kusimamia utendaji katika kuandaa na kutekeleza mpango wa manunuzi, ripoti ya fedha, ukaguzi na kazi kamati za menejimenti za Wizara.

97. **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 2,004,294,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Utumishi na Uendeshaji, kati ya fedha hizo **Shilingi 1,233,899,000** ni Mishahara na **Shilingi 770,395,000** ni kwa Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## PROGRAMU NDOGO YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI

98. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti ina lengo la kuratibu kazi za Mipango Sera na Utafiti kwa maendeleo ya sekta ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi. Programu ndogo hii itatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Programu Ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo;

    i. Kufanya tafiti za kiuchumi na kijamii kwa mujibu wa agenda ya Utafiti ya Zanzibar na kuchapisha matokeo ya tafiti hiyo.

ii. Kushirikiana na Ofisi ya Mtakwimu mkuu wa Serikali katika ukusanyaji na usambazaji wa Takwimu.

iii. Kushirikiana na Tume ya Mipango katika Kuandaa na kufanya tathmini ya utekelezaji wa miradi pamoja na kusimamia miradi ya Wizara itakayotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

iv. Kuandaa Mpango kazi, bajeti ya Wizara na Ripoti za Utekelezaji kwa kila robo mwaka.

v. Utekelezaji wa kazi za kamati za kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

vi. Kufanya Ufuatiliaji wa Programu / Miradi ya Maendeleo kwa kila robo mwaka.

vii. Kuandaa miradi mipya ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi pamoja na kuratibu usimamizi wa miradi inayoendelea ya wizara.

viii. Kuratibu vikao vya Mashirikiano ya Wizara kwa SMT na SMZ pamoja na mashirikiano ya ndani, kikanda na kimataifa.

ix. Kuratibu kazi ya uandaaji wa Sheria, Kanuni na Miongozo mbalimbali ya Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

**99. Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 493,145,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti. Kati ya fedha hizo **Shilingi 140,982,000** ni Mishahara, na **Shilingi 352,163,000** ni Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

**PROGRAMU NDOGO YA URATIBU NA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI PEMBA**

**100. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba ina lengo la kuratibu maendeleo ya Uchumi wa Buluu

na uvuvi. Programu ndogo hii inatoa huduma za utumishi za Wizara; kuwajengea uwezo wa kitaaluma watumishi na kuratibu kazi za mipango za Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi.

**101.** **Mheshimiwa Spika,** Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, Programu hii inalenga kutekeleza shabaha zifuatazo:

i. Kuratibu vikao vinne (4) na ziara za kamati ya Utalii, Biashara na Kilimo katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa malengo ya Wizara Pemba.

ii. Kufanikisha ziara za viongozi wa Wizara kitaifa.

iii. Ufuatiliaji na utekelezaji wa kazi za Wizara na Taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi Pemba.

iv. Kuimarisha mashirikiano na Taasisi nyenginezo za Serikali, Sekta binafsi na Taasisi za kijamii.

**102.** **Mheshimiwa Spika,** naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha matumizi ya jumla ya **Shilingi 1,220,049,000** kwa ajili ya Programu ndogo ya Uratibu wa Ofisi Kuu Pemba kwa matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo **Shilingi 1,011,107,000** ni Mishahara na **Shilingi 208,942,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Uendeshaji wa Ofisi.

## MUHTASARI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

**103.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, imekadiriwa kukusanya mapato ya jumla ya **Shilingi 5,921,734,000** kupitia vianzio vyake vitano vya Unguja na Pemba.

**104.** **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, inaomba kuidhinishiwa

